# 18. NDOTO YA NEBUKADREZA

*“Hakika Mungu wenu ndiye Mungu wa miungu na Bwana wa wafalme, awezaye kufumbua siri"*

## Shabaha

Kuonyesha namna Mungu alivyombariki Danieli na rafiki zake katika Babeli na akawafunulia maana ya ndoto ya Nebukadreza.

Nebukadreza, mfalme, alichukua mateka wengi sana kila aliposhuka na kuja kupigana na ufalme wa Yuda. Miongoni mwa mateka wa mwanzo, alikuwa ni Daniel na rafiki zakewatatu, Hanania, Mishaeli, Azaria. Mfalme alikusudia **“awafundishe elimu na lugha ya Wakaldayo”** kwa sababu aliona kuwa walikuwa vijana wenye maarifa na wenye kufahamu elimu. Kwa njia hii alitaka kuondoa kabisa mawazo ya imani yao ya Mungu waliyemwabudu katika Yuda na akawashawishi waabudu na kuheshimu miungu ya Babeli.

Hata hivyo, hakuamini, kuwa mateka hawa vijana walikuwa ni watu wenye ufahamu mkubwa wa imani ambo walikuwa wako tayari kufa kuliko kumwacha BWANA, Mungu wao.

Danieli 1 na 2

## DANIELI NA RAFIKI ZAKE WANAPEWA JARIBIO: Danieli 1:3-21

Kama sehemu yake ya kuwashawishi wafalme vijana ili wawe waabuduo miungu ya Babeli, mfalme Nebukadreza alibadilisha majina yao na akawaita kwa mjina ambayo yanaheshima kwa miungu ya Babeli. Kisha akaamuru wapewe kila siku chakul a na divai kutoka katika meza ya mfalme. Danieli na rfiki zake walitambua kuwa chakula hicho na divai viliwekwa kwanza wakfu kwa miungu ya mfalme, maana hiyo ndiyo iliyokuwa desturi ya nchi ya Babeli. Wao wakamwambia msimamizi mkuu awapatie mtama (maharagwe na dengu) na maji badala ya chakula cha mfalme. Akimwongopa mfalme, asije kujulikana kuwa hakutii agizo lake hatimaye akakubali kuwaweka katika majaribio kwa muda siku kumi. Na baada ya siku kumi ilikuwa ni dhahiri kwa watu wote kuwa Danieli na rafiki zake walikuwa na **“nyuso zao zilikuwa nzuri zaidi na miili yao ilikuwa imenenepa zaidi”** kuliko vijana wote ealiokula chakula cha mfalme (mstari 15). Mungu akawajalia kupata kibali na huruma machoni pa huyu mtumishi wa mfalme kwa sababu ya uaminifu wa utii kwa Mungu. Na ingawa walikuwa katika nchi za watu asiomjua Mungu, wakiwa mbali na nchi ambayo Mungu aliwapatia baba zao, vijana hawa waliendelea kumwabudu Mungu wao, naye akaendelea kuwabariki, **“akiwapatia maarifa na ujuzi katika elimu na hekima: Danieli naye alikuwa na ufahamu katika maono yote na ndoto”** (mstari 17)

## NDOTO YA NEBUKADREZA: Danieli 2

Usiku mmoja, mfalme Nebukadreza aliota ndoto ya kubwa sana na ya kushangaza na ya kutisha.Ilimhangaisha sana, hata asiweze kulala usingizi tena.Aliwaita wote wenye hekima ili waweze kumwambia ndoto kwa kuwa alidhamiria kujua maana ya ndoto hiyo inayotisha sana.Ikawa wenye hekima walipokuja walimwambia mfalme, **“Tuonyeshe sisi watumishi wako ile ndoto, nasi tutakuonyesha ile tafsiri yake”** (mstari 4). Nebukadreza aliwafahamu watu wake hao wenye hekima kuwa wana akili sana, na hakutaka kusikiliza maelezo yoyote ya kuvutia kugeuza kusudi la nia yake. Alitaka kujua kweli. Alikataa kuwajulisha ndoto yake. Na hii ilionekana kwao kuwa ni jambo lisilowezekana. Ni njia gani gani wangeweza kujua ndoto ya mfalme aliyoota kitandani mwake / Hata hivyo mfalme hakubadilisha nia yake. Wamwambie ndoto na tafsiri yake ama wafe. Walilalamika, **Hapana mtu duniani awezaye kulionyesha neno hili la mfalme; kwa maana hapana mfalme wala bwana, wala liwali, aliyetaka neno kma hili wala hapana mwingine awezye kumwonyesha mfalme neno hilo, ila miungu, wasio na kikao pamoja na wenye mwili”** (mstari 10-11)

Mfalme akagadhabika sana, akatoa amri ya kuwaangamiza wenye hekima wote-**“wakawatafuta Danieli na wenzake ili wauawe”** (mstari 13).

Danieli aliposikia amri ya mfalme ya kuwaua wote,alimwomba mkuu wa walinzi, **“mbona amri hii ya mfalme ina ukali namna hii”** (mstari 15). Mkuu wa walinzi akamwambia sababu, Danieli mara moja akamwomba muda na atamwezesha mfalme kufahamu yote mawili ndoto

na tafsiri ya ndoto hiyo. Kwa hiyo Danieli na rafiki zake watatu wakmwomba Mungu awafunulie ile ndoto ya mfalme. Mungu akasikia maombi yao, akamwonyesha Danieli yote mawili, ndoto namaana ya ndoto. Danieli, akaingia kwa mfalme Nebukadreza kwa kujiamini sana.

Danieli, akasema, **“yuko Mungu mbinguni afunuaye siri, naye amemjulisha mfalme Nebukadreza mambo yatakayokuwa siku za mwisho”** (mstari 28).

## DANIELI ANAIFUNUA NDOTO: Danieli 2:31-35

Katika yake, mfalme aliona sanamu kubwa sana mbele yake. Ilikuwa na uzuri wa ajabu na ilikuwa na mwangaza sana na kuonekana kwake kulikuwa kwa kutisha sana.

**KICHWA cha sanamu** kilikuwa cha **DHAHABU safi**

**TUMBO** na **MIKONO** ilikuwa ya **FEDHA**

**TUMBO** na MAPAJA ilikuwa ya **SHABA**

**MIGUU** ilikuwa ya **CHUMA**

**NYAYO** zilikuwa ni za **CHUMA na UDONGO**

Na alipokuwa akitazama aliona jiwe, **“lilichongwa mlimani bila kazi ya mikono”** likipiga sanamu kwenye nyayo likaivunja sanamu vipande vipande. Na kwa kuwa nyayo zilipondwapondwa na sanamu yote ili anguka na kupondekapondeka. Sanamu yote ikawa imevunjika vunjika na upepo ukavipeperusha **“vikawa kama makapi ya viwanja vya kupepetea wakati wa hari”** (mstari 35). Lile jiwe lililoipiga sanamu hiyo likaongezeka, likaongezeka hata likawa mlima mkubwa sana likaijaza dunia yote.

## TAFSIRI YA NDOTO: Danieli 2:37-45

Na hii ndiyo iliyokuwa ndoto ya Nebukadreza na Danieli akaendelea kumjulisha mfalme maana ya ndote yake yote. **Mungu wa mbinguni amekupa ufalme, na uwezo, na nguvu, na utukufu,”** Danieli akamweleza, **“wewe u kichwa kile cha dhahabu”** (mstari 37, 38). Madini mengine manne yaliyofuata yaliwakilisha falme nne ambazo zingefuata baada ya ufalme wa Babeli.

**FEDHA** inasimama baada ya **UMEDI-UAJEMI**

**SHABA** inasimama baada ya ,**UYUNANI**

**CHUMA** inasimama baada ya **RUMI**

**CHUMA na UDONGO**

inawakilisha Ulaya iliyogawanyika.Ambapo leo tunaona baadhi ya nchi zina nguvu za kijeshi na zingine ni dhaifu.

Sanamu iliyosimama mbele zake iliwakilisha FALME ZA WANADAMU, maana kila utawala ulioonyeshwa katika sanamu ulikuwa ukitawali na wanadamu ambao hawakumjua kabisa au hawakumtii Mungu wa mbinguni. Wote walikuwa wagumu wa mioyo, wakatili na wapenda vita. Nia yao kubwa katika maisha yao ilikuwa ni kujiwezesha wao wenyewe kuwa na nguvu za kijeshi na utajiri, kwa kuyafanya maisha ya maelfu ya watu wanaotawaliwa kuwa ya umaskini na mateso kutoka kwa wanowatawala.

Leo tunaishi katika siku za mwisho za ufalme wa wanadamu.Uovu wa aina hiyo ulionekana katika ufalme wa zamani wa wanadamu, unaendelea kuonekana katika miongoni mwa viongozi siku hizi. Hawa wote ni watu wasiomcha Mungu wanaofurahia kutumia nguvu dhidi ya watu wengine na sifa na nyadhifa zao.

## NGUVU ZA JIWE: Danieli 2:44-45

Jiwe linawakilisha nini? Lilikuwa ni dogo mwanzo, lakini linapiga nyayo za chuma na udongo na kusababisha sanamu yote kuharibika. **Nguvu za JIWE** zinawakilisha **UFALME WA MUNGU.**

Bwana Yesu Kristo atarudi kuangamiza falme za wanadamu. Kwanza kabisa atayaangamiza majeshi ya mataifa yote, ambayo yatakuwa yamekuja katika nchi ya Israeli kupigana na Yerusalemu (Zekaria 14:2). Kuanzia hapo ufalme wake utaongezeka mpaka utaijaza dunia yote. Ufalme huo utaanzishwa baada ya kuangamizwa kwa mataifa yote ya duniani.

Tofauti na Ufalme wa wanadamu, Ufalme wa Mungu utakuwa na mfalme mwenye busara na wa haki akitawala kwa kicho cha Mungu (2 Samweli 23:3). Atakuwa mwenye haki mwenye huruma na atawajali sana masikini na wahitaji.

(Zaburi 72 maelezo ya uzuri ajabu wa mfalme atakayetawala ufalme wa Mungu). Ulimwengu utakuwa na amani wakati wanadamu wote watakapomtii Mungu na mwisho dunia yote taijawa na utukufu wa Mungu (Isaya 9:6-7;11:9).

Hili litatokea lini? Danieli aliweza kueleza kuwa mambo haya yote yatapita katika siku ambazo sanamu yote itakuwa imesimama juu ya nyayo zake za chuma na udongo.

**"Na katika siku za wafalme hao Mungu wa mbinguni atausimamisha ufalme, ambao hautaangamizwa milele, wala watu wengine hawataachiwa enzi yake; bali utavunja falme hizi zote vipandevipande na kuziharibu, nao utasimama milele na milele"** (Danieli 2:44).

## FUNDISHO KWETU

Ndoto ailiyomsumbua sana Nebukadreza ni ya muhimu sana kwetu kwasababu inazungumzia mambo ya siku zetu, inaelekea chini kabisa ukianzia kwenye kichwa cha dhahabu mpaka wakati wa nguvu za Jiwe zitakapofunuliwa.Na siku yoyote sasa Bwana Yesu Kristo anaweza kutokea. Yeye mwenyewe alitupatia maneno ya kututahadharisha: **"Kesheni basi; kwa maana hamujui ni siku ipi atakayokuja Bwana wenu"** (Mathayo 24:42). Yesu anatutaka sisi kuendelea kuwa waaminifu kwake, ili kwamba tuweze kumsaidia kuubadilisha ulimwengu uwe mahali pa kuishi penye utukufu na furaha.

## MASWALI

### Majibu Mafupi

1. Nebukadreza alitaka awafundishe nini Danieli na rafiki zake waliokuwa utumwani?
2. Ni kwa nini Nebukadreza alibadilisha majina ya Daniele na rafiki zake?
3. Ni kwa nini walikataa chakula cha mfalme?
4. Waliomba wapewe nini badala yachakula cha mfalme?
5. Ni jinsi gani Mungu aliwabariki Danieli na rafiki zake?
6. Ni kwa nini Nebukadreza alikataa kuwapatia wenye hekima ndoto yake?
7. Wenye hekima wlimwambia nini mfalme baada ya kukataa kuwapatia ndoto yake?
8. Danieli alijuaje ndoto aliyoota mfalme?
9. Ilitokea nini kwa sanamu baada yajiwe kuipiga kwenye nyayo za chuma na udongo?
10. Je jiwe linawakilisha nini?
11. Ni nani atakayeziangamiza falme za wanadamu?
12. Ufalme wa wanadamu utawekwa wapi?

### Majibu ya Kina

13. Fafanua ndoto aliyoota Nebukadreza?
14. (a) Eleza jiwe liliifanyaje sanamu?
    (b) Ni nini kiliitokea sanamu?
    (c) Eleza ni jambo gani litalitotokea Jiwe baada ya hapo?
15. (a) Eleza ufalme wa wanadamu unafanana na?
    (b) Onyesha ni jinsi ufalme wa Mungu utakavyokuwa tofauti

16. Angalia picha ya sanamu aliyoiona Nebukadreza na andika:
   (a) Kila sehemu ilikuwa imetengenezwa kwa?
   (b) Kila sehemu inawakilisha utawala upi?
   (c) Chora Jiwe katika mchoro wako na onyesha lilifanya nini na linamwakilisha nani?

